**SHERIA YA BENDERA YA ZANZIBAR, NEMBO YA SERIKALI, WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR NA WIMBO MAALUMU YA MWAKA 2017**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**BENDERA YA ZANZIBAR**

3. Bendera ya Zanzibar.

4. Matumizi ya Bendera ya Zanzibar.

5. Yaliyo marufuku kwa Bendera ya Zanzibar.

**SEHEMU YA TATU**
**NEMBO YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

6. Nembo ya Serikali.

7. Matumizi ya Nembo ya Serikali.

8. Yaliyo marufuku kwa Nembo ya Serikali.

**SEHEMU YA NNE**
**WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR**

9. Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

10. Matumizi ya wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

11. Yaliyo marufuku kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

## SEHEMU YA TANO
## WIMBO MAALUMU WA UKOMBOZI NA KUWAENZI MASHUJAA

12. Wimbo maalumu.

13. Yaliyo marufuku kwa Wimbo maalumu.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

14. Kukashifu Bendera ya Zanzibar.

15. Kukashifu Nembo ya Serikali.

16. Kukashifu Wimbo wa Taifa.

17. Kukashifu Wimbo Maalumu.

18. Adhabu ya Jumla.

19. Uwezo wa Waziri kuondoa au kupunguza masharti.

## SEHEMU YA SABA
## MENGINEYO

20. Uwezo wa Waziri Kutunga Kanuni.

21. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAMBA 2 YA 2017**

**NIMESAINI**

**{DK. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

28 Machi, **2017**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA NEMBO NAM. 1 YA 1985 NA SHERIA YA BENDERA YA ZANZIBAR NAM. 12 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI BORA YANAYOHUSIANA NA BENDERA YA ZANZIBAR, NEMBO YA SERIKALI, WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR NA WIMBO MAALUMU YA 2017 NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu ya mwaka 2017 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Kinachofanana" inajumuisha picha au kinachofanana na picha, mchoro, maandishi au muziki, uchoraji wa kutumia rangi au aina yoyote ya upatikanaji wa vitu vinavyofanana na hivyo iwe kwa umbo au ukubwa au kwa namna nyengine yoyote kinyume na Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu;

"Nembo ya Serikali" maana yake ni Muhuri wa Serikali kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika kifungu cha 3(1) ambapo katika Sheria hii itajulikana kama Nembo ya Serikali;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Wimbo Maalumu" maana yake ni kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 12 cha Sheria hii.

"Bendera ya Zanzibar" maana yake ni Bendera ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Wimbo wa Taifa wa Zanzibar" maana yake ni wimbo wa Taifa wa Zanzibar uliotajwa katika kifungu cha 9 cha Sheria hii;

## SEHEMU YA PILI
## BENDERA YA ZANZIBAR

Bendera ya Zanzibar.

**3.** Kutakuwa na Bendera ya Zanzibar itakayokuwa na maelezo kama yalivyotolewa katika Jadweli la kwanza la Sheria hii.

Matumizi ya Bendera ya Zanzibar.

**4.** Bendera ya Zanzibar itatumika katika maeneo ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria na katika maeneo yatakayotangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Yaliyo marufuku kwa Bendera ya Zanzibar.

**5.** Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar au mfanano wake katika mambo yafuatayo:

(a) kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kinachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza;

(b) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza, kuzalisha inayouzwa au inayotolewa kwa ajili ya mauzo;

(c) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza au kuzalisha, kwa mtu kufanya hivyo kinyume na madhumuni yaliyoidhinishwa na Waziri;

(d) katika kuboresha matangazo au matangazo kwa ajili ya biashara yoyote, viwanda au taaluma;

(e) kama nembo ya chama cha siasa;

(f) kama mapambo au mambo ya sanaa;

(g) kuchapishwa zaidi kwa neno au picha; au

(h) kwa namna yoyote au sehemu iliyokatazwa kisheria.

## SEHEMU YA TATU
## NEMBO YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Nembo ya Serikali.

**6.**(1) Kutakuwa na Nembo ya Serikali kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 3 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

(2) Nembo ya Serikali itakuwa na itachukuliwa kwamba ni kielelezo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na itatumika kwa madhumuni ya Serikali pekee.

(3) Nembo ya Serikali maelezo yake ni kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

Matumizi ya Nembo ya Serikali.

**7.** Nembo ya Serikali itatumika katika maeneo ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria.

Yaliyo marufuku kwa Nembo ya Serikali.

**8.** Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia Nembo ya Serikali au mfanano wake katika mambo yafuatayo :

(a) kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kinachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza;

(b) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza, kuzalisha inayouzwa au inayotolewa kwa ajili ya mauzo;

(c) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza au kuzalisha, kwa mtu kufanya hivyo kinyume na madhumuni yaliyoidhinishwa na Waziri;

(d) katika kuboresha matangazo au matangazo kwa ajili ya biashara yoyote, viwanda au taaluma;

(e) kama nembo ya chama cha siasa;

(f) kama mapambo au mambo ya sanaa;

(g) kuchapishwa zaidi kwa neno au picha; au

(h) kwa namna yoyote au sehemu iliyokatazwa kisheria.

## SEHEMU YA NNE
## WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

Wimbo wa Taifa wa

**9.**(1) Kutakuwa na wimbo wa Taifa wa Zanzibar ambao maelezo yake ni kama ilivyoelezwa katika Jadweli la tatu la Sheria hii.

(2) Wimbo wa Taifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utakuwa katika mfumo wa maandishi au muziki au vyote viwili.

Matumizi ya wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

**10.** Wimbo wa Taifa wa Zanzibar utatumika katika maeneo ambayo matumizi yake hayana vikwazo kwa mujibu wa sheria.

Yaliyo maru-fuku kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

**11.** Ni marufuku kwa Mtu yeyote kufanya yafuatayo kwa Wimbo wa Taifa wa Zanzibar:

(a) kubadilisha uhalisia wake;

(b) kutumia katika kuboresha matangazo au matangazo kwa ajili ya biashara yoyote, viwanda au taaluma; au

(c) kuuimba na kuutumia katika maeneo yasiyokubalika kisheria;

## SEHEMU YA TANO
## WIMBO MAALUMU WA UKOMBOZI NA KUWAENZI MASHUJAA

Wimbo maalumu.

**12.**(1) Kutakuwa na wimbo maalumu wa Ukombozi na kuwaenzi mashujaa wa Zanzibar ambao maelezo yake ni kama ilivyoelezwa katika Jadweli la nne la Sheria hii.

(2) Wimbo maalumu utatumika kujenga hamasa za uzalendo kwa Zanzibar na utaimbwa katika skuli zote za Zanzibar na maeneo mengine yatakayoainishwa katika Sheria hii au Sheria nyengine.

(3) Matumizi mengine na sauti yatakuwa kama yatakavyoainishwa katika Kanuni.

Yaliyo maru-fuku kwa Wimbo maalumu.

**13.** Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo kwa Wimbo Maalumu:

(a) kubadilisha uhalisia wake;

(b) kuutumia katika kuboresha matangazo au matangazo kwa ajili ya biashara yoyote, viwanda au taaluma; au

(c) kuimba na kuutumia katika maeneo yasiyokubalika kisheria;

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

Kukashifu Bendera ya Zanzibar.

**14.** Mtu yeyote atakaefanya kitendo chochote au kubadilisha lolote au kuchapisha kinyume na Sheria hii Bendera ya Zanzibar au mfanano wake kwa nia ya kuikashifu au kuidharau au kuikejeli au yanayofanana na hayo, ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua fedha za Tanzania Shilingi milioni moja na si zaidi ya Shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kukashifu Nembo ya Serikali.

**15.** Mtu yeyote atakaefanya kitendo chochote au kubadilisha neno lolote au kuchapisha kinyume na Sheria hii Nembo ya Serikali au mfanano wake kwa nia ya kukashifu au kudharau au kukejeli au yanayofanana na hayo, ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua fedha za Tanzania Shilingi milioni moja na si zaidi ya Shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kukashifu Wimbo wa Taifa.

**16.** Mtu yeyote atakaefanya kitendo chochote au kubadilisha neno lolote au kuchapisha maandishi yoyote au kuupiga au kuuimba Wimbo wa Taifa au mfanano wake kinyume na Sheria hii kwa nia ya kukashifu au kudharau au kukejeli au yanayofanana na hayo, ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua fedha za Tanzania Shilingi milioni moja na si zaidi ya Shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kukashifu Wimbo Maalumu.

**17.** Mtu yeyote atakaefanya kitendo chochote au kubadilisha neno lolote au kuchapisha maandishi yoyote au kuuimba au kuupiga Wimbo Maalumu au mfanano wake kinyume na Sheria hii kwa nia ya kukashifu au kudharau au kukejeli au yanayofanana na hayo, ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua fedha za Tanzania Shilingi milioni moja na si zaidi ya Shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Adhabu ya Jumla.

**18.** Mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria hii kwa adhabu ambazo hazijaainishwa, atatozwa faini isiyopungua fedha za Tanzania Shilingi laki tano na si zaidi ya Shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Uwezo wa Waziri kuondoa au kupunguza masharti.

**19.**(1) Waziri anaweza kuondoa au kupunguza masharti chini ya vifungu vya 5,8,11 na 13 vya Sheria hii kwa kuzingatia makubaliano na masharti kwa kadri atakavyoona inafaa, na kwa maandishi, kwa mtu yeyote, au kikundi cha watu, kwa kitu chochote, aina ya vitu vyovyote au masharti ya marufuku yaliyotajwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mtu atakaekwenda kinyume na makubaliano ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la jinai na ikithibitika atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki tano na si zaidi ya Shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

## SEHEMU YA SABA
## MENGINEYO

Uwezo wa Waziri Kutunga Kanuni.

**20.**(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri uwezo wa jumla wa Waziri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni mahsusi katika masuala yanayohusiana na:

(a) ukubwa wa vipimo, rangi na uwiano wa bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali.

(b) Vipimo vya ala za sauti na maandishi ya Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalum;

(c) Uchanganuzi wa watumiaji wa Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu;

(d) Uchanganuzi wa matukio yanayostahiki kutumika kwa Bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali;

(e) Nidhamu na heshima ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu;

(f) Matumizi ya Bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali katika majengo ya Serikali na binafsi;

(g) Matumizi ya Bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali katika sare za Idara Maalum;

(h) Matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu katika michezo;

(i) Kuweka katika nyaraka rasmi na machapisho;

(j) Itifaki ya Bendera na Nembo ya Serikali;

(k) Matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalumu katika Skuli za Umma na Skuli za binafsi;

(l) Utafutaji na ukamataji;

(m) Vyombo vya mawasiliano vya kielektroniki;

(n) Kuweka Bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali pamoja na Bendera na Nembo ya Serikali nyengine;

(o) Kuweka Bendera ya Zanzibar na Nembo ya Serikali pamoja na Bendera na Nembo zisizokuwa za Kitaifa;

(p) Gwaride na sherehe;

(q) Nusu mlingoti;

(r) Katika uchapishaji na uzalishaji; na

(s) Uondoshaji.

(3) Waziri hatoweza kutunga Kanuni chini ya kifungu kidogo cha (2) (a) na (b) cha kifungu hiki bila ya kupata ridhaa ya Baraza la Mapinduzi.

Kufuta na kubakiza.


**21.**(1) Sheria ya Nembo Namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Namb. 12 ya 2004 zinafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa au hatua iliyochukuliwa chini ya masharti ya Sheria zilizofutwa, itachukuliwa imefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA
**{Chini ya kifungu cha 3}**

## BENDERA YA ZANZIBAR

Bendera hii ina muundo wa mstatili na imegawanyika katika sehemu tatu zilizo lala sawa; sehemu ya chini ni kijani (ikionyesha ardhi ya Zanzibar), sehemu ya katikati ni nyeusi (ikionyesha rangi ya watu wa Zanzibar) na sehemu ya juu ni buluu isiyokoza (ikionyesha bahari na mawingu yaliyoizunguka Zanzibar); na kuingizwa Bendera ya Tanzania juu ya upande wa kushoto. Vilevile Bendera ina utepe mweupe upande wa kushoto kutoka juu hadi chini ya bendera hiyo (inayoashiria amani).



## JADWELI LA PILI
**{Chini ya kifungu cha 6}**

## NEMBO YA SERIKALI

Nembo ya Serikali ya Zanzibar ina sura ya mviringo ambayo imebeba mnazi upande wa kushoto na Mkarafuu upande wa kulia, visiwa viwili vya Zanzibar (Unguja na Pemba) ambavyo vipo katikati ya mviringo, eneo la ardhi na bahari lililobeba miti. Taji lipo juu ya mviringo ndani yake lina maneno "SMZ". Mviringo umeshikiliwa na Shoka upande wa kushoto na Panga upande wa kulia. Chini ya mviringo kuna kikalio chenye maneno "SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR.

**JADWELI LA TATU**
**{Chini ya kifungu cha 9}**

**WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR**

Mungu ametubarikia, Unguja na Pemba yote

Sote tunashangiria, Jamhuri kutuletea.

Mungu ametubarikia, Unguja na Pemba yote.

**JADWELI LA NNE**
**{Chini ya kifungu cha 12}**

**WIMBO MAALUMU**

Sisi sote tumegomboka, kwa ndugu zetu walopotea
Walopigania nchi yetu, makusudi ya kuigomboa
Hatusahau maisha yetu, kwa roho zao walozitoa

Ndugu zetu wamepotea, kwa kugombania nchi yetu
Muhanga wao wamejitoa, kwa kulilinda Taifa letu
Kwa roho zao walozitoa, hatusahau maisha yetu

Hao ndio walimu wetu, waliokwisha kujitolea
Na sisi hatutorudi nyuma, sote mbele tutaendelea
Kwa kulilinda Taifa letu, muhanga sote twajitolea

Umepitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 17 Februari, 2017.

**(RAYA ISSA MSELLEM)**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**